Toleo 69 - Rabi-ul Awal 1444 H / Oktoba 2022 M

Jarida la UQAB

**TAARIFA KWA VYOMBO VYYA HARABI**
Mamlaka ya Palestina Inaendelea kutekeleza Dori ya Uvamizi katika Umwagaji damu ya Wapalestina

**HABARI NA MAONI**
Chaguzi Za Kidemokrasia: Njia Ya Kumakinisha Ukoloni Mamboleo

**MATOLEO**
Je! Utawala wa Kifalme Utaweza Kubakia Hai?

**JIBU LA SWALI**
Uchaguzi wa Urais Nchini Kenya



# ZIMBABWE INAHITAJI MABADILIKO YA KIMSINGI KUTOKANA NA MFUMO WA KIBEPARI NA SIO SARAFU PEKEE

**Afisi ya Habari Ardhi ya Baraka Palestina**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

KUMB: 02/1444 Jumanne, 24 Safar 1444 H 20/09/2022 M


**Taarifa kwa Vyombo Vya Habari**

# Mamlaka ya Palestina Inaendelea kutekeleza Dori ya Uvamizi katika Umwagaji damu ya Wapalestina

Kwa kushirikiana na umbile la Kiyahudi na uhali wake, vikosi vya Mamlaka ya kihalifu ya Palestina (PA) huko Nablus, jana usiku, tarehe 9/19/2022, walitekeleza uhalifu wao mbaya wa kumuua kijana Firas Yaish na kuwajeruhi wengine kadhaa, wakati wa uwakandamizaji wao wa waandamanaji wanaopinga kukamatwa kwa Mujahidina Musab Shtayyeh na Brigedia Jenerali Tabila ambao wanatafutwa na umbile la Kiyahudi wakati huo huo vikosi vya uvamizi vilikuwa vikikamata watu katika miji ya Ukingo wa Magharibi, na walowezi walikuwa wakivamia Mji wa Mkongwe wa Hebron wakiwa na ulinzi wa jeshi lao. Chomb cha PA kilikuwa kikitekeleza dori yao ya kufedhehesha, ya udanganyifu, na chafu walilokabidhiwa katika kuwaandama mujahidina na kuwaua watoto wa Palestina.

Mamlaka ya Palestina yalijitolea jinai yake kwa kulitumikia umbile la Kiyahudi kukataa udhaifu wake na kushindwa kutekeleza dori yake katika kulinda usalama wake, na kwa Hussein al-Sheikh, Majed Faraj na Ziad Hab al-Rih kuthibitisha kwamba wako tayari kutumia huduma za usalama kwa kazi zote chafu kwa niaba ya uvamizi.

Kwa upande mwingine, vyombo vya PA ni viziwi, mabubu na vipofu wa mauaji, mashambulizi, na uhalifu wa kila siku huko Jenin, Nablus na miji mingine yote ya Palestina yanayotekelezwa na umbile la Kiyahudi. Na kwa sababu hawana heshima wala uungwana, hawakukerwa na mauaji ya mashujaa na kupigwa mabomu na kubomolewa nyumba wakazi wao!

Kuielezea Mamlaka ya Palestina kuwa ni mzigo kwa watu wa Palestina sio maelezo sahihi tena, bali imekuwa ni njama hatari na yenye maangamivu kwa kadhia ya Palestina. PA imelenga maisha ya watu kupitia sera zake za kiuchumi zinazofukarisha watu, imefanya kazi katika kutekeleza sera za ushuru ili kufadhili ufisadi wake na kudumisha usalama wa umbile la Kiyahudi. Mamlaka ya Palestina imefungua milango wazi kwa sheria za taasisi na shughuli za ufisadi na kwa sheria zilizoingilia moja kwa moja chombo cha familia. Pia imedhamiria kuwatia nguvuni wale wanaoendeleza ulinganizi wa mema na ukatazaji maovu na wale wote wanaotahadharisha watu kuhusu njama za kikoloni za Kimagharibi. Mamlaka ya Palestina ni mradi wa kuisalimisha kwa haraka na kuibomoa kadhia ya Palestina na hii ndio iliyokuwa misheni yake tangu kutiwa saini kwa Makubaliano ya Oslo hadi sasa. Imefanya kazi na bado inafanya kazi kuvunja utashi wa watu na kuitokomeza nafsi yoyote ambayo bado ina fahari na hamu ya kupambana. Pia inafanya kazi ya kuzima moto wa jihad na upinzani kwa mvamizi, huku ikiwapotosha watu katika mpango wake wa kupata dola dhalilifu kwa mujibu wa azimio la Marekani la dola mbili na kila mtu anajua kwamba haya ni mangati ya udanganyifu.

**Watu wa Ardhi Iliyobarikiwa:** Mamlaka ya Palestina na viongozi wake sio sehemu ya lengo lenu bali ya ni adui yenu. Yale ambayo umbile la Kiyahudi imepata kupitia Mamlaka ya Palestina yasingewezekana bila ya usaliti na njama zake. Misheni yake ni kutokomeza ari ya mapambano ndani yenu na kuangamiza familia zenu ili Mayahudi wanyakuzi waishi kwa usalama katika ardhi hii iliyobarikiwa.

Kwa damu tukufu inayomwagwa na umbile la Kiyahudi kila siku nchini Palestina, imedhihirika wazi kwamba PA inafanya kazi kwa maslahi yake binafsi, na sio kwa maslahi yenu au ya lengo lenu.

Usaliti wa utawala wa Palestina na tawala zote zinazouzunguka na pia wale walio mbali nao umedhihirika.

Mbele ya ukweli wote huu, imebakia njia moja tu ya wokovu ambayo ni kuunganisha taifa na lengo lake na kufanya kazi ya kuregesha Khilafah inayounganisha Ummah na kuling'oa umbile la Kiyahudi na tawala zote zinazolilinda. Hapo ndipo hadhi, usalama na dini vitahifadhiwa, Palestina itakombolewa na Al-Aqsa itaregea kwa wamiliki wake halali, kwa Umma wa Kiislamu.

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Ardhi Iliyobarikiwa – Palestina**

# HABARI NA MAONI
# Chaguzi Za Kidemokrasia: Njia Ya Kumakinisha Ukoloni





**Habari:**

Baada ya IEBC kumtangaza naibu rais Dkt William Ruto kuwa ndiye rais –mteule, ujumbe wa maseneta wa Amerika ukiongozwa na Seneta Chris Coons uliizuru Kenya. Ikumbukwe kwamba seneta Chris alikua mchangiaji mkubwa sana wa mazungumzo ya 'handshake' kati ya rais Uhuru Kenyatta na aliekuwa waziri mkuu wa Raila Omolo Odinga.

**Maoni:**

Ujumbe huu uliokutana na viongozi muhimu serikalini kiuhakika unahitaji kumulikwa kwa kina na kuangaliwa kwa umakini mkubwa. Kwa upande mwengine, balozi wa Uingereza nchini Kenya, Jane Marriot kwenye mtandao wake wa Twita akaandika kwamba: 'Uingereza haiungi mkono au kupendekeza mgombea au chama chochote katika uchaguzi huu.

Marekani na Uingereza kuingilia mchakato wa kisiasa wa Kenya unaonesha wazi mapambano na kinyang'an'ganyiro kwa mataifa ya ulimwengu wa tatu ili ziendelee kuwekwa chini ya ushawishi na mduara uleule wa mabeberu wa kikoloni.Na hili ndilo linaloangaliwa zaidi na mataifa haya.

Ukoloni kama sera ya kigeni ya mataifa ya kimagharibi hujaalia chaguzi za Kidemokrasia zinabakia kuwa ni zana na uwanja kwa mapambano na kinyang'ang'anyiro kwa rasilimali za ulimwengu wa tatu.

Mataifa ya kimagharibi ya Kibepari yameweza kutunga urongo wa madaraka na uhuru ambao hata huwahadaa wasomi miongoni mwa wananchi. Hakika Demokrasia inabaki na itaendelea kuwa njia ya kikoloni kudumisha ukoloni mamboleo.

Sisi katika Hizb ut-Tahrir twapenda kueleza kinagaubaga kwamba walimwengu hawatoweza kujikomboa kutoka pingu za ukoloni ispokuwa kupitia kusimamisha Uislamu kimfumo na kiserikali.


**Imeandikwa kwa ajili ya Ofisi kuu ya Habari ya Hizb ut-Tahrir na**

**Ali Omar Albeity**
**Mwanachama wa Ofisi ya Habari Hizb ut-Tahrir Kenya.**

# HABARI NA MAONI

# Zimbabwe Inahitaji Mabadiliko ya Kimsingi Kutokana na Mfumo wa Kibepari na Sio Sarafu Pekee

**Habari:**

Benki Kuu ya Zimbabwe hivi karibuni imezindua sarafu mpya ya dhahabu inayoitumainia kutokamana nayo itapunguza mahitajio ya pesa za kigeni. Katika uzinduzi rasmi wa sarafu hiyo jijini Harare, John Mangudya, Mkuu wa Benki Kuu ya Akiba nchini Zimbabwe alithibitisha kuwa sarafu hiyo itatumika kupunguza mahitajio ya dolari za Marekani nchini humo.

**Maoni:**

Zimbabwe ni nchi iliyokoloniwa na kupata uhuru wake wa bendera mwaka 1980. Tangu uvamizi na ukoloni wa Afrika kutoka kwa mabepari wamagharibi wenye kiu ya damu mwishoni mwa karne ya 19, Zimbabwe imekuwa chini ya ushawishi wa Uingereza mpaka leo na hili ni tatizo lake la msingi linalopaswa kutatuliwa, kwa kuondoa kabisa ukoloni mamboleo.

Zimbawe inatabikisha mfumo muovu wa kiuchumi wa kibepari ambao ndio chanzo kikuu cha majanga na mashaka yote ya kiuchumi yanaoikumba. Zaidi ya hapo, sera za uchumi wa kibepari zimepelekea mporomoko wake huku uchumi wake ukisinyaa kwa 6% mwaka 2019 na 10% mwaka 2020.

Kwa mujibu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika, mgogoro wa kiuchumi umefanya mfumko wa bei kuwa sehemu ya uchumi wa Zimbabwe, ukipanda na kufikia 222.9% mwaka 2019 na 622.8% mwaka 2020, nakisi ya bajeti iliongezeka kutoka 2.7% mwaka 2019 hadi 2.9% mwaka 2020. Thamani ya ubadilishaji wa fedha za kigeni ilishuka na kuwa ZWL2.5 Februari 2019 na kujaribu kuimarika kwa ZWL82 kwa dolari ya Marekani Disemba 2020. Umasikini ulifikia 70.5% mwaka 2019 huku ukosefu wa ajira ukiendelea kukua kwa 21% .

Kutokana na kufungwa minyororo ya mashirika ya fedha ya kimataifa kama Mfuko wa Fedha wa Kimataifa(IMF), deni jumla la Zimbabwe ni dolari bilioni 11.1 (53.9% ya pato la taifa), ambalo 95.6% ni madeni ya nje, ambayo ni pamoja na dolari bilioni 6.4 nakisi ya marejesho kwa taasisi za fedha za kimataifa, nchi wahisani na wakopeshaji binafsi.

Katika hali hii, umasikini umekuwa ni sehemu ya maisha ya watu wa Zimbabwe kama matokeo ya sababu tulizozitaja hapo awali. Kuzinduliwa kwa sarafu mpya ya dhahabu kunawatia mashaka wataalamu wa masuala ya uchumi na watu wa kawaida nchini Zimbabwe kuhusu ufanisi wake. Prosper Chitambata, Mtafiti Mwandamizi na Mwanauchumi katika Taasisi ya Maendeleo ya Utafiti wa Kazi na Uchumi ya Zimbabwe, alisema: "Hata mahitaji ya dolari ya Marekani yataongezeka…watu wengi hawatakuwa na uwezo wa kununua sarafu hizi kwani watu wengi wanaishi kwa kipato cha kijungu mwiko" Hii ni kwa sababu gharama za sarafu moja ya dhahabu ni $1,800 ambapo kwa mfanyikazi wa kawaida wa serikali anayelipwa $180 hadi $200 kwa mwezi atalazimika kukusanya mishahara yake ya miezi kumi au mwaka mzima ili aweze kununua sarafu moja!

Sarafu ya dhahabu ni sehemu ya pesa za Kiislamu katika mfumo wake wa kiuchumi, kudumisha kiwango cha dhahabu na fedha lilikuwa ni jambo lililokuwepo katika kipindi chote chini ya Khilafah, na kwa hilo uchumi wa ulimwengu ulikuwa imara kwa karne 13. Uislamu pia unakomesha uchumi wa kinyonyaji, unakataza riba, benki za kinyonyaji, masoko ya hisa, ambayo kiujumla mambo kama haya hudhoofisha mfumo halisi wa uchumi katika mzunguko wa fedha.

Kwa muktadha wa Zimbabwe, inatarajiwa kwa kuanzishwa kwa sarafu mpya ya dhahabu hakutabadilisha chochote, kwani sarafu ni kiraka kimoja tu, ilhali mfumo mzima wa uchumi na siasa bado ni wa kibepari ambao ndio unaoendesha na kusimamia mambo ya watu ukitumia ukoloni kama njia ya kunyonya rasilimali za Zimbabwe na kutia umasikini watu na nchi. Kwa hiyo, kama kutakuwa hakuna mabadiliko ya kimfumo, mabadiliko ya sarafu ya dhahabu hayatafanya kazi na kuleta matunda yaliyokusudiwa.

Inachopaswa Zimbabwe kujua ni kuwa, ili viwango vya dhahabu viweze kufanya kazi ipasavyo panahitajika mfumo wa uchumi wa Kiislamu ambao nao pia hauwezi kufanya kazi isipokuwa pale ambapo Uislamu unatekelezwa kama mfumo katika nyanja zote za maisha chini ya serikali ya Kiislamu ya kiulimwengu (Khilafah).

Tunatoa mwito kwa watu wa Zimbabwe na nchi zinazoendelea kiujumla kuwa muda umefika wa kuachana na ubepari uliotuletea majanga yasiyoelezeka kwa wanadamu. Pia tunawakumbusha watu wa Zimbabwe haswa, kuwa Uislamu ndiyo uliyowapelekea ustaarabu katika karne ya 15 kutokea Afrika Mashariki na Msumbiji kupitia biashara na kuoana baina ya Waislamu na watu wa kabila la Shona, hali iliyopelekea kustawi kwa ufalme wa Mutapa na kukuwa kwa miji kama Salisbury (Harare) ikiwa na historia ya muda mrefu na utajiri katika uchimbaji wa dhahabu. Yote haya yalimalizwa baada ya uvamizi na ukoloni wa Kireno na baadaye Uingereza.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Said Bitomwa**

**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania**

# Je! Utawala wa Kifalme Utaweza Kubakia Hai?

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Adnan Khan**



Kifo cha Malkia Elizabeth II kimeifanya Uingereza kuingia katika kipindi cha maombolezi ya pamoja. Upeperushaji mpana wa mazishi na utawala wa malkia wa miongo saba umeshughulisha watu. Kumekuwa na mihemko na rambirambi kutoka kote ulimwenguni huku wengi wakimuona Malkia Elizabeth II kama mtu thabiti katika siasa za Uingereza. Nyumba ya Kifalme ya Windsor leo ndio familia ya kifalme iliyohudumu kwa muda mrefu zaidi na Malkia Elizabeth II alikuwa mfalme aliyehudumu kwa muda mrefu zaidi, utawala wake ulihusisha mawaziri wakuu 15, kuanzia Winston Churchill na kumalizia na Liz Truss, ambaye Elizabeth alimteua kuwa waziri mkuu mnamo Septemba 6. Huku enzi ya Elizabeth inapofika mwisho, enzi ya Mfalme Charles III inaanza; changamoto kubwa kwa Nyumba ya Kifalme, kando na aibu zake nyingi za mara kwa mara, sio tu kuhifadhi uhalali wake, bali jinsi taasisi ya zamani ya zama za kati inabaki kuwa muhimu katika ulimwengu wa kisasa.

Malkia Elizabeth amepokea sifa nyingi kwa kujitolea kwake katika kazi na kwa kuwa kipengee maarufu cha maisha ya kisiasa ya Uingereza. Amekuwa mtu ambaye anaonekana kutoa utulivu wakati maisha ya kisiasa ya Uingereza yanasuasua sana. Lakini je, kazi ya Familia ya Kifalme ni nini? Kwa baadhi, kazi ya Familia ya Kifalme ni kuunga mkono mfumo wa kidhalimu ili kuwazubaisha watu kutokana na hali halisi za maisha yao kwa gwaride na ibada. Kwa wengine, ufalme ni ishara Waingereza wanaweza kuungana karibu ambao pia hutoa utulivu na ni mwongozo kwa serikali. Ilhali kwa baadhi ya wengine, ufalme wa kisasa ni aina ya nguvu laini, inayotoa taswira ya kitaifa kwa ulimwengu na kuwavutia wageni, kutembelea kama watalii. Wanafamilia wa hivi karibuni zaidi, kama vile Kate Middleton na Meghan Markle (ambaye alikuwa Binti Mfalme wa Sussex hadi alipokiacha cheo chake cha kifalme) kuingia ndani ya Familia ya Kifalme wameonekana na wengi kama ushindi wa nguvu laini kwa Uingereza. Kazi ya Ufalme wa Uingereza sio kama ilivyokuwa zamani licha ya mamia ya miaka ya historia. Familia ya kifalme ya Uingereza imeweza kubakia hai katika eneo na enzi ambapo fadhila za urithi ni jambo lililopitwa na wakati.

Historia ya Ulaya ya Zama za Kati inajumuisha wafalme wenye kutawala sehemu kubwa za bara hilo wakiwa wameungana na Kanisa la Kikristo baada ya kuporomoka kwa Himaya ya Kirumi katika karne ya 5. Kufuatia uvamizi na makaazi ya Viking katika karne ya 9, Ufalme wa Anglo-Saxon wa Wessex uliibuka kama ufalme mkuu wa Kiingereza. Alfred Mtukufu aliipata Wessex, akapata mamlaka juu ya Mercia magharibi na kujitwika cheo 'Mfalme wa Waingereza.' Mjukuu wake alikuwa mfalme wa kwanza kutawala juu ya ufalme wa muungano uliokaribiana na mipaka ya sasa ya Uingereza. Hawa wafalme wa Anglo-Saxon waliingia katika Ukristo na Askofu Mkuu wa Canterbury angempaka mfalme mafuta matakatifu, akimuinua mfalme juu ya kila mtu mwengine. Kuanzia wakati huu hadi katikati ya karne ya 17 Wafalme wa Uingereza walitawala.

***Endelea... UK 6***

Kufikia mwisho wa karne ya 18 kutelekezwa kwa ufalme wa Uingereza nchini Amerika na mapinduzi ya umwagaji damu nchini Ufaransa mnamo 1789 yalikuwa yamezipa falme jina baya. Demokrasia, utawala wa uwakilishi na dola za kitaifa yalikuwa ndio mlipuko. Ulimwengu ulikuwa unabadilika na utawala wa kifalme ulionekana kama kitu cha zama katili zilizopita.

Mwanzoni mwa karne ya 20, falme na himaya nyingi kuu za ulimwenguni zilipinduliwa. Qajar nchini Iran, Qing nchini China, Habsburgs nchini Austria na Hohenzollerns nchini Ujerumani zote zilifikia mwisho. Ufalme wa Uingereza ulibadilika na kujirekebisha. Malkia Victoria alitoka katika Nyumba ya Kifalme ya Kijerumani ya Saxe-Coburg na Gotha na mwanawe mkubwa, Mfalme Edward VII, alichukua jina la makaazi ya kila mara ya familia ya majira ya kiangazi katika vitongoji vya magharibi mwa London - Windsor, mnamo 1917, kwa sababu ya chuki dhidi ya Wajerumani wakati wa Vita vya Kwanza vya Dunia (WW1).

Kuporomoka kwa Uingereza kama dola ya kiulimwengu baada ya Vita vya Pili vya Dunia (WW2) kuliipa Familia ya Kifalme sababu mpya ya kuendelea kuwepo. Maafisa wa Uingereza walitumia maonyesho yote yaliyozunguka Familia ya Kifalme kama njia ya kuitangaza Uingereza kote ulimwenguni na kwa nadharia Malkia alikuwa mkuu wa nchi kwa mataifa na maeneo kadhaa. Familia ya kifalme ilikuja kuunda nguvu laini ya Uingereza katika enzi ambayo nguvu ngumu ya Uingereza ilikuwa ikipungua. Dori ya wanaufalme ilihusisha kusafiri mara kwa mara kwa Jumuiya ya Madola na zaidi ya kutoa medali, vyeo vya Himaya ya Uingereza na kuhudhuria sherehe na hafla za michezo kama ishara ya mamlaka ya Uingereza. Huku enzi ya baada ya WW2 ikiwavaa wale waliohusisha nembo ya kitaifa na ufalme walikuwa wakizidiwa na kizazi kipya ambacho kiliuona ufalme kama taasisi ya zama za kati.

Serikali mtawalia za Uingereza zimeitumia Familia ya Kifalme kama nembo ya taifa, rai jumla imekuwa ikiongezeka ya kuondolewa kwa ufalme. Hii ni kwa sababu utawala wa kifalme unakwenda kinyume na mambo mengi ya maisha ya kisasa. Ufalme kutokana na uzawa una nafasi ya upendeleo nchini, kamwe hawakuchaguliwa. Huku wengi wakiiona familia ya kifalme kama chanzo cha kiburi, kashfa za mara kwa mara zimeharibu sifa zao. Talaka, mahusiano ya pembeni, kukwepa kodi, kuondoka kwa Meghan Markle na Mwanamfalme Harry kama wanafamilia ya kifalme wanaofanya kazi na tuhuma za unyanyasaji wa kijinsia na ubakaji dhidi ya Mwanamfalme Andrew: yote yameharibu vibaya sana sifa ya Familia ya Kifalme. Ingawa uungaji mkono wa umma kwa Malkia Elizabeth ulikuwa wa juu kama 60%, maoni kwa wanafamilia wengine wa kifalme yamekuwa ya chini na yanaendelea kupungua na hii inaiweka Nyumba ya Windsor katika hali mbaya baada ya kufariki Malkia Elizabeth II.

Malkia Elizabeth aliweza kuuweka ufalme kuwa muhimu kwa kutabanni na kuweka dori ya wanafamilia ya kifalme kwani falme zingine ziliondolewa au kupinduliwa kwa nguvu. Wanasiasa wa Uingereza pamoja na tabaka tawala la Uingereza wanaiona Familia ya Kifalme kupitia macho ya kiuchumi na nguvu laini ambayo huleta uaminifu na watalii nchini Uingereza. Malkia Elizabeth aliweza kuendeleza utamaduni wa enzi za kati kutoa taswira ya ufahari, umoja na kitambulisho cha kitaifa kwa Uingereza. Lakini kwa kufariki Malkia na huku Mfalme Charles akichukua dori la ubwana, ufalme wa Uingereza unakabiliwa na kazi kubwa sana ya kuweka taasisi ya zamani za kati na ya kiurithi kuwa muhimu.

# Hukmu za Uislamu kuhusiana na Jinsia, Jinsia Isiyofahamika, na Kubadili Jinsia



**Utangulizi: Mdahalo juu ya Ulinzi wa Watu Waliobadili Jinsia katika Ulimwengu wa Kiislamu**

Mnamo tarehe 5 Septemba 2022, Seneta wa Pakistan Mushtaq Ahmad aliwasilisha mswada wa marekebisho katika Sheria ya Kuwalinda Wanaobadili Jinsia, 2018, kwa Kamati ya Kudumu ya Seneti ya Haki za Kibinadamu. Katika mkutano huo, Seneta Mushtaq Ahmad, alisema kuwa, "Transgender ni neno la Kimarekani, halina nafasi katika Uislamu, na sheria kuhusu jamii ya watu waliobadili jinsia ni kinyume na Qur'an na Sunnah na itakuza ushoga." Mjadala mpana kuhusu ulinzi wa watu waliobadili jinsia, umekuwa mada ya mkanganyiko ndani ya Ulimwengu wa Kiislamu. Imewaongoza hata wachache kutilia shaka uhalali wa Uislamu katika zama hizi.

Ili Waislamu wazungumze na kutenda kulingana na yale yanayomridhisha Mwenyezi Mungu (swt), ni muhimu kuyaweka mambo yanayohusu jinsia katika mapali pake sahihi. Uislamu unawataka Waislamu wachunguze suala (mas'alah) hilo kisha wachukue hatua kwa mujibu wa hukmu za Shariah kuhusiana na suala hilo. Hivyo basi Waislamu nawachunguze uamuzi wa kijinsia kwa kuzingatia sifa za kibiolojia, za kimwili pamoja na za kihisia, kwa kuzingatia jeni, kazi za jinsia za jinsia isiyoeleweka na mtazamo wa dume jike au jike dume, pamoja na mabadiliko ya homoni na ubadilishaji jinsia kupitia upasuaji.

**Ujinsia ni Fahamu ya Kimagharibi ya Kufafanua Jinsia kupitia Mtazamo wa Kibinafsi**

Magharibi imetabanni mtazamo mpya kuhusu suala la jinsia katika miongo ya hivi karibuni. Ili kutibu karne nyingi za ubaguzi wa kikatili dhidi ya wanawake, kutokana na Kanisa la Kikristo na itikadi zake za ukandamizaji, Magharibi iligeukia "ujinsia" ili kufafanua jinsia. Magharibi iliipa mgongo fahamu ya jinsia, kwa mujibu wa kipimo cha uwili wa kibaolojia, yaani uume na uke, badala yake wakageukia fahamu ya ujinsia. Chini ya ujinsia, jinsia hufafanuliwa kulingana na muundo wa kithaqafa na kijamii wa mtu binafsi. Chini ya ujinsia, jinsia hupeanwa kupitia fikra za mtu binafsi, kwa mtazamo wa kibinafsi, na si kwa biolojia. Kama mwanafalsafa wa Kifaransa wa filosofia ya uwepo huru wa mtu binafsi, Simone de Beauvoir, alivyosema, "Mtu hazaliwi, lakini badala yake anakuwa, mwanamke (Kifaransa: On ne naît pas femme, on le devient)" katika kitabu chake 'Jinsia ya Pili' (Kifaransa: Le Deuxième Sexe).

Ujinsia, asili, uliibuka kama sehemu ya wimbi la pili la utetezi wa haki za wanawake, katika jitihada za kuondoa ubaguzi wa kijinsia, kwa kuzingatia uwili wa uume na uke. Kwa hivyo, ujinsia ulitaka kuondoa uamuzi wa kibaolojia wa jinsia. Kwa kufanya hivyo, ujinsia pia ulitaka kuondoa matokeo yake, unyanyapaa wa kijinsia na dori za kijinsia, ambayo yalionekana kuwa ya kukandamiza.

**Ujinsia Umetabanniwa na Vuguvugu la Ushoga**

Kiasili, ujinsia ulitabanniwa ili kuzuia ubaguzi dhidi ya wanawake, na wanaume. Hata hivyo, ujinsia ukapanuliwa kutoka kwa uungaji mkono haki za wanawake, hadi uungaji mkono haki za mashoga. Ujinsia iliungwa mkono kwa kiasi kikubwa na watetezi wa ushoga, ili kukomesha ubaguzi, dhidi ya wale wanaojitangaza kuwa mashoga. Kwa hivyo, lengo la ujinsia halikufungika tena tu katika kukomesha ubaguzi dhidi ya wanawake. Ujinsia ulipanuliwa ili kukomesha ubaguzi dhidi ya wale waliojichagulia jinsia, kupitia mtazamo wao wa kibinafsi, bila kujali sifa za kibaolojia.

Kupitia fahamu yake ya uhuru wa kibinafsi, Magharibi iliruhusu watu binafsi kujipachika jinsia, kwa namna wanavyojitazama kibinafsi. Kwa hivyo, kulingana na ujinsia, mwanamume anaweza kuamua kuwa yeye

***Endelea... UK 8***

ni mwanamke, licha ya ukweli kwamba ana sifa za kibaolojia za mwanaume. Anaweza kufanyiwa upasuaji na tiba ya homoni ili kubadili jinsia aliyojichagulia. Kwa hivyo mtu aliyebadili jinsia anaweza kuficha sifa za kibaolojia za kiume na kupata sifa za kibaolojia za kike. Watu waliobadili jinsia ambao hutumia usaidizi wa kimatibabu kubadilisha jinsia zao, kwa njia hii, wanaitwa 'transsexual'. Vile vile, mwanamke anaweza kujiona kuwa yeye ni mwanamume. Kisa maarufu ni cha mwanamke, Ellen Paige, ambaye aligeuka kuwa Elliot Page, baada ya mabadiliko ya upasuaji na homoni. Kwa hiyo, sasa katika mtazamo wa Kimagharibi kuna watu waliobadili jinsia (transgender), ambao wana kitambulisho cha kijinsia, tofauti na jinsia yao ya kibaiolojia wakati wa kuzaliwa.

Kwa upande wa Sheria ya Ulinzi ya Watu Wanaobadili Jinsia ya Pakistan, baada ya kufanyiwa marekebisho, imeegemezwa juu ya fikra ya ujinsia ya Kimagharibi. Inasisitiza, "Mtu aliyebadili jinsia atakuwa na haki ya kutambuliwa kulingana na kitambulisho chake wa kijinsia kupitia anavyojitazama mwenyewe." Kwa hivyo kulingana na watawala wa Pakistan, jinsia inapaswa kuamuliwa kwa kujitazama kibinafsi, kama watetezi wa Magharibi, badala ya kuzingatia baolojia peke yake, kama Uislamu unavyo taka.

**Muamala wa Uislamu kwa Jinsia na Dori ya Kijinisa**

Mwenyezi Mungu (swt) anasema,

**[وَلَيْسَ الذَّكَرُ كَالْأُنثَىٰ]**

**"Na mwanamume si sawa na mwanamke."** [Surah Aali Imran 3:36]. Katika Uislamu, kiasili kuna jinsia mbili. Jinsia hizi mbili huamuliwa na masuala ya kibiolojia pekee. Jinsia haiamuliwi na uamuzi wa mtu binafsi au mtazamo wa kibinafsi. Jinsia isiyoeleweka inaamuliwa na wataalamu, kama moja ya jinsia mbili. Kisha, dori za kijinsia zinaamuliwa na Sharia iliyoteremshwa kwa wahyi na Mwenyezi Mungu. Katika Uislamu, kuna hukmu za Shariah kwa wanadamu wote, wanaume na wanawake, na pia kuna hukmu za Shariah ambazo ni maalum za kijinsia. Kwa hiyo, Uislamu uliwapa majukumu wanaume pamoja na wanawake kuhusiana na Swalah, Saumu, Hijja na Zaka. Kisha, Uislamu ukatoa hukmu za Shariah kwa mwanamke peke yake, kuhusu hedhi, mimba na uzazi wa mtoto. Uislamu pia ulimpa mwanamke haki ya ulezi wa watoto, kando na mwanamume. Uislamu ulimpa mwanamke haki ya kuchuma, ambapo mume wake hana haki katika mali yake, huku ukimlazimu mwanamume kumpa masrufu mke wake na watoto wake. Kupigana si faradhi kwa wanawake, ilhali ni faradhi kwa wanaume.

Kuepusha kuleta ukandamizaji juu ya mwanamke, au mwanamume, Shariah inahakikisha kwamba wanaume na wanawake wanashirikiana, ili kuzalisha familia imara na jamii yenye utulivu inayoegemezwa kwenye kitengo hicho. Hata bila ya Khilafah ili kuzuia dhulma na ufisadi, maisha ya familia katika Ulimwengu wa Kiislamu yanasalia kuwa mwenge, kwa wale walioko Magharibi, wanaokabiliwa na matokeo mabaya, ya uharibifu wa maisha ya familia.

**Uislamu Huipa Jinsia Isiyoeleweka (خُنْثَى Khuntha) Jinsia kutoka katika Jinsia Mbili**

Neno 'khuntha' linatumika kwa mtu ambaye hawezi kujulikana kwa urahisi, kuwa ni mwanamume au mwanamke, kwa mazingatio ya kibiolojia. Ni mwanadamu ambaye ana maumbile ya kiume na ya kike, au yule ambaye hana yoyote. Katika Uislamu, mtaalamu humpa yule aliye na jinsia isiyoeleweka moja ya jinsia mbili, mwanamume au mwanamke, baada ya kutafiti uhalisia wa kibaolojia. Mwanafaqihi wa kale Ibn Qudamah alisema katika kitabu chake Al-Mughni, kuhusiana na utata: "Haitengwi kuwa ya kiume au ya kike. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

**[وَأَنَّهُ خَلَقَ الزَّوْجَيْنِ الذَّكَرَ وَالأُنْثَى]**

**"Na kwamba Yeye ndiye aliye umba jozi, dume na jike."** [Surah An-Najm 53:45]. Na Yeye (swt) amesema,

**[وَبَثَّ مِنْهُمَا رِجَالا كَثِيرًا وَنِسَاءً]**

**"Na akaeneza kutokana na wawili hao wanaume na wanawake wengi."** [Surah An-Nisaa 4:1] na kwa hivyo hakuna kiumbe cha tatu."

Kwa hivyo, Uislamu haujaweka jinsia ya tatu. Daktari muaminifu wa Kiislamu ambaye ni mtaalamu wa masuala ya dosari katika uume na uke, maumbile ya kijinsia, jeni na tabia ya kijinsia, huthibitisha jinsia. Kwa hivyo yeye, kwa utulivu na umakini, huchunguza kwa undani tabia za kibaolojia, za kimaumbile, za kimwili, kwanza, ili kuona ni kipi kinachotawala, cha sifa za kiume au za kike. Yeye huchunguza mambo ya kimwili, kama vile sehemu za siri, na pia kuzingatia kromosomu za jinsia za X na Y, zinazounda jinsia. Ikiwa, katika hali nadra sana, kwamba sifa za kimaumbile na za kijeni pekee hazitatui utata, suala la kibaolojia ya kiume na kike, mivutio ya kijinsia na hamu pia huzingatiwa, kabla ya kuamua jinsia. Baada ya hapo, hukmu za Kiislamu hutumika kulingana na jinsia iliyoamuliwa, ikiwemo ndoa, dori na majukumu ya kijinsia.

Mara tu uamuzi wa kijinsia unapokuwa umefanywa, unaidhinishwa na amri ya Khalifah, kama mamlaka ya Waislamu, ambaye ni lazima atiiwe. Baada ya hapo, mtu huyo anaamiliwa na jamii pana, kulingana na jinsia aliyopewa, bila ya ubaguzi. Mwanamume au mwanamke ameunganishwa kama mwanajamii anayethaminiwa wa jamii ya Kiislamu, ili kwamba majukumu yote ya Shariah yaweze kutekelezwa, huku haki zote za Shariah zikitolewa.

**Hukmu ya Uislamu Kuhusiana na Mwanamume**

*Endelea... UK 9*

**Mwenye Kujifananisha na Mwanamke (مُخَنَّث Mukhannath) na Mwanamke Mwenye Kujifananisha na Mwanamume (مُتَرَجِّلَةُ Mutarajillah)**

Ibn Abbas (ra) amesimulia, «لَعَنَ رَسُولُ اللَّهِ صلى الله عليه وسلم الْمُتَشَبِّهِينَ مِنَ الرِّجَالِ بِالنِّسَاءِ، وَالْمُتَشَبِّهَاتِ مِنَ النِّسَاءِ بِالرِّجَالِ» **"Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amewalaani wanaume wanaojifananisha na wanawake, na wanawake wanaojifananisha na wanaume."** [Bukhari]. Ibn Abbas (ra) amesimulia kwamba, «لعن الله الْمُخَنَّثِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالْمُتَرَجِّلَاتِ مِنَ النِّسَاءِ وَقَالَ أخرجوهم من بُيُوتكُمْ» **"Mwenyezi Mungu amewalaani wanaume wanaojifananisha na wanawake, na wanawake wanaojifananisha na wanaume, na akasema watoeni majumbani mwenu."** [Bukhari]. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) amesema, «ثَلَاثَةٌ لاَ يَنْظُرُ اللَّهُ عَزَّ وَجَلَّ إِلَيْهِمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ الْعَاقُّ لِوَالِدَيْهِ وَالْمَرْأَةُ الْمُتَرَجِّلَةُ وَالدَّيُّوثُ» **"Watu watatu Mwenyezi Mungu Mtukufu hatawatazama Siku ya Kiyama: Mwenye kuwaasi wazazi wake wawili, na mwanamke mwenye kujifananisha na wanaume na Dayuthi."** [An-Nisaa]

Kujifananisha na jinsia huja kwa maana jumla, katika upande wa kitambulisho, tabia, mavazi na suluki. Inakuja kwa maana kamili, bila ya mipaka na tofauti yoyote. Dhambi inaenea hadi kwenye mahusiano ya kimwili, na jinsia moja, na yote yanayopelekea katika hilo. Kwa hivyo, katika Uislamu, matamanio na vivutio sio mwamuzi wa kitendo. Badala yake, hukmu za Shariah ndio huamua mahusiano kati ya wanaume na wanawake, pamoja na mwenendo, tabia na dori zao. Baada ya Uislamu kuamua namna ya mahusiano, kwa undani, mapenzi na mahusiano ya kimwili hutukia ndani ya fungamano la ndoa, kati ya mwanamume na mwanamke. Ni Khilafah ndiyo itakayozalisha mazingira yanayokuuza dori sahihi za kijinsia. Jamii ya Kiislamu ndiyo iliyo mbali sana na mkanganyiko, taabu na mateso haya ambayo hadhara ya Kimagharibi imesababisha kupitia uhuru na dhihirisho lake, ujinsia.

**Mtazamo wa Uislamu juu ya Ubadilishaji Jinsia**

Jinsia haiamuliwai kwa kujitazama kibinafsi, na kupuuza uhalisia wa kibaolojia wakati wa kuzaliwa. Kubadilisha jinsia ya mtu kutoka kwa mwanamume kwenda kwa mwanamke, au kinyume chake, kunachukuliwa kuwa ni kubadilisha uumbaji wa Mwenyezi Mungu ﷻ ambao umeharamishwa. Hii ni ima mabadiliko hayo yanatokana na tiba ya kihomoni au upasuaji. Amesema Mwenyezi Mungu (swt):

[إِن يَدْعُونَ مِن دُونِهِ إِلَّا إِنَاثًا وَإِن يَدْعُونَ إِلَّا شَيْطَانًا مَّرِيدًا (117) لَّعَنَهُ اللَّهُ ۘ وَقَالَ لَأَتَّخِذَنَّ مِنْ عِبَادِكَ نَصِيبًا مَّفْرُوضًا (118) وَلَأُضِلَّنَّهُمْ وَلَأُمَنِّيَنَّهُمْ وَلَآمُرَنَّهُمْ فَلَيُبَتِّكُنَّ آذَانَ الْأَنْعَامِ وَلَآمُرَنَّهُمْ فَلَيُغَيِّرُنَّ خَلْقَ اللَّهِ ۚ وَمَن يَتَّخِذِ الشَّيْطَانَ وَلِيًّا مِّن دُونِ اللَّهِ فَقَدْ خَسِرَ خُسْرَانًا مُّبِينًا (119) يَعِدُهُمْ وَيُمَنِّيهِمْ ۖ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا]

**"Wao hawawaombi badala yake Yeye ila wanawake, wala hawamuombi ila Shet'ani aliye asi (117) Mwenyezi Mungu amemlaani. Naye Shet'ani alisema: Kwa yakini nitawachukua sehemu maalumu katika waja wako (118) Na hakika nitawapoteza na nitawatia matamanio, na nitawaamrisha, basi watakata masikio ya wanyama, na nitawaamrisha, basi watabadili aliyo umba Mwenyezi Mungu. Na mwenye kumfanya Shet'ani kuwa ni mlinzi wake badala ya Mwenyezi Mungu, basi huyo amekhasiri khasara ya dhaahiri (119) Anawaahidi na anawatia tamaa. Na Shet'ani hawaahidi ila udanganyifu (120)"** [Surah An-Nisaa 4:117-120].

Katika suala la mpito wa mwanamume hadi mwanamke, ni kudhihirisha sifa za uke, au kuficha sifa za uume. Hata hivyo, haibadilishi uhalisia wa kibaolojia wa mtu huyo wakati wa kuzaliwa, ambao ndio msingi wa uwekaji wa jinsia katika Uislamu. Kwa hivyo hukmu za asili ya jinsia yake zinabaki kuwa za kiume, kabla ya mabadiliko. Haijuzu kwa mwanamume mwengine kufanya mkataba wa ndoa na mtu wa asili ya kiume, bila ya kujali mabadiliko hayo.

**Hitimisho: Kukabiliana na Batili ya Fikra ya Ujinsia**

Baada ya kuhakikisha uharibifu wa familia na maadili ya familia katika nchi zao, Magharibi inafanya kazi kupitia watawala wa Waislamu kutangaza vita vya kithaqafa dhidi ya Uislamu na Waislamu. Katika Magharibi, serikali za Kimagharibi zina uwezo wa kuongoza na kudhibiti watu wao kwa urahisi, kutokana na kusambaratika kwa familia na kusababisha ukosefu wa mshikamano, jamii na hatua za pamoja. Watawala wa nchi za Magharibi sasa nao wanataka vivyo hivyo kwa Waislamu, kwa kuwa wameshindwa kukabiliana na Uislamu kifikra na kiitikadi. Sasa hivi inaeneza fikra ya ujinsia miongoni mwa Waislamu ili kuwafisidi, ikitaka kuangamiza mfumo wa kijamii na mafungamano imara ya kifamilia miongoni mwa Waislamu. Hii ni ili Magharibi iweze kuwadhibiti Waislamu, kuzuia, au angalau kuchelewesha, mwamko wa Ummah kupitia Khilafah kwa Njia ya Utume. Ni juu ya Waislamu kukabiliana na wimbi hili la ufisadi kupitia kujijenga imara kithaqafa kutoka kwenye Uislamu, huku wakifanya kazi ya kusimamisha tena ngao yao ya ulinzi, Khilafah.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Musab Umair – Wilayah Pakistan**

 

# JIBU LA SWALI

# Uchaguzi wa Urais Nchini Kenya

**Swali:**

(Kiongozi wa upinzani nchini Kenya, Odinga, mnamo Jumatatu: “22/08/2022,” aliwasilisha rufaa rasmi katika Mahakama ya Upeo kuhusu matokeo ya uchaguzi wa urais alioshinda mpinzani wake, William Ruto, Naibu Rais anayemaliza muda wake. Shirika la Associated Press liliripoti kwamba Odinga aliwasilisha nyaraka za kupinga leo asubuhi kwa Mahakama ya Upeo ambayo yalazimika kujibu ndani ya kipindi cha siku 14 kulingana na sheria... 22/08/2022, Shirika la Anadolu). Mnamo Agosti 15, 2022, alitangazwa kwamba William Ruto alimshinda mpinzani wake Odinga kwa tofauti ndogo katika uchaguzi wa urais uliofanyika nchini Kenya mnamo Agosti 9, 2022... Katika kampeni hizi za uchaguzi, Rais Kenyatta alionekana kumpinga naibu wake, William Ruto, na kumuunga mkono hasimu wake, kiongozi wa Upinzani Odinga baada ya maridhiano kufanyika kati yao. Je, huu ulikuwa ni mchezo wa Kenyatta kuonyesha kwamba anamuunga mkono mpinzani wake Odinga na kumpinga naibu wake, Ruto, ili kumhakikishia ushindi naibu wake dhidi ya mpinzani wake? Nini siri ya hatua za Amerika kwa Kenya? Je, kuna mgogoro kati yake na Uingereza?

**Jibu:**

Ili kufafanua jibu la maswali ya hapo juu, tunawasilisha mambo yafuatayo:

1- Angazo letu kwa Kenya ni kuwa ni sehemu ya eneo la Pembe ya Afrika, ambayo inachukuliwa kuwa eneo la Kiislamu lenye umuhimu wa kimkakati na kiuchumi. Watu wengi wa eneo hilo ni Waislamu na walitawaliwa na Uislamu. Nchi hizi zina mafungamano ya wao kwa wao na wengi wao walikuwa chini ya mabavu ya ukoloni wa Waingereza. Kenya ilikuwa imefungamanishwa na Sultan Muislamu wa Zanzibar hadi ilipoangukia chini ya utawala wa kikoloni wa Muingereza mwishoni mwa karne ya kumi na tisa. Licha ya kuwa Kenya ilipata uhuru wake tangu mwisho wa 1963, lakini huo ulikuwa ni uhuru bandia, kwani uhusiano wake na Uingereza ulionekana kupitia mawakala, Utawala wake ulifuatiwa na mawakala wa Uingereza tangu Jomo Kenyatta kutoka uhuru wakati wa uhuru bandia hadi 1978 kwenda kwa Daniel arap Moi hadi 2002, kwenda kwa Mwai Kibaki hadi 2013, hadi alipokuja Uhuru Kenyatta, mtoto wa rais wa kwanza Jomo Kenyatta. Na akashinda tena katika uchaguzi wa 2017. Uingereza inaunda mawakala kwa macho pevu kutoka kwa baba hadi watoto na mikononi mwa watawala mawakala ambao hawampi mamlaka yeyote isipokuwa akiwa ni kibaraka wa aina yao, na wa jinsia ya wasaidizi wao na uaminifu wao kwa mkoloni mwenyewe...

2- Amerika iliweza kujimakinisha katika kuchuma mawakala kutoka kwa upinzani, haswa Odinga, ambaye kabila lake linachukuliwa kuwa kabila la tatu nchini, na kwa sababu hii nchi ilianza kushuhudia mapambano ya kikoloni ya kisiasa ambayo yanachukua muondoko wa kikabila. Vyama vyake vinachukuliwa kuwa vya kikabila, na vinapata uungwaji mkono wa wafuasi wa makabila yake kwa jumla. Uhusiano wa kikabila ndio kiungo kati ya wanachama wa chama kimoja. Kila ulipofanyika uchaguzi, damu ilimwagika kupinga matokeo yao, kwa kasumba ya mtoto wa kabila letu. Naye William Ruto, rais mpya aliyetangazwa ushindi katika uchaguzi wa hivi majuzi, anatoka makabila ya Wakalenjin anayotoka Rais wa zamani Daniel arap Moi. Na Ruto anajivunia kuwa mwanafunzi wa rais huyu wa zamani, baada ya kujiunga na chama chake tangu mwaka wa 1992.

3- Matokeo rasmi yalitangazwa, huku Ruto akishinda kwa tofauti ndogo, kwani alipata 50.5%, huku Odinga akipata 48.8% ya kura. Itambuliwe kuwa kuna mgawanyiko ndani ya Tume ya Huru ya Uchaguzi, na mkuu wa tume ya uchaguzi, Wafula Chebukati, alisema: "Tumefunga safari ili kuhakikisha kuwa Wakenya wanapata uchaguzi huru, wa haki na wa kuaminika, na safari hii haikuwa rahisi," huku naibu wake, Juliana Cherera, akisema, "Hatuwezi kupitisha matokeo yatakayotangazwa kutokana na hali ya kutoeleweka ya awamu hii ya mwisho ya uchaguzi mkuu" (BBC 15/8/2022). Makamishna wanne kati ya saba wa tume ya uchaguzi yenyewe walikataa kutambua matokeo haya, na kuibua tuhuma za udanganyifu. Kulikuwa na maandamano kupinga matokeo. Odinga alisema: "Ili kuepusha mashaka, ningependa kusisitiza kwamba tunakataa kata kata na kutoridhika na matokeo ya urais yaliyotangazwa jana na Bw. Chebukati" (Anatolia 8/16/2022) na amekwenda katika Mahakama ya Upeo kwa rufaa rasmi mbele ya Mahakama ya Upeo. Shirika la habari la Amerika la ‘Associated Press’ lilisema kuwa "Odinga aliwasilisha asubuhi ya leo (tarehe 22 Agosti 2022) karatasi za pingamizi kwenye Mahakama ya Upeo, ambayo lazima ijibu ndani ya siku 14 kwa mujibu wa sheria." Na iwapo mahakama itakubali rufaa hiyo, uchaguzi utarudiwa ndani ya siku 60 kwa mujibu wa sheria, na hilo halitatengwa hadi wapinzani wanyamazishwe kwa sababu tofauti ni ndogo sana kati ya pande hizo mbili na kwa sababu Tume ya Uchaguzi imegawanyika, na ili kusiwepo vitendo vya vurugu na misukosuko ya matokeo mabaya, inaufanya upinzani uwe na matumaini ya kushinda duru ya pili iwapo hilo litatangazwa au kuwekwa itifaki juu ya muundo wa maridhiano kati ya pande hizo mbili kama kumpa Odinga uwaziri mkuu baada ya kuundwa mara nyengine tena!

4- Kama ilivyo desturi, upinzani hudai udanganyifu katika uchaguzi unaposhindwa, hasa nchini Kenya wakati upinzani huu ni wa Marekani na mshindi ni kutoka kwa mawakala wa Uingereza, na kinyume chake hutokea katika nchi nyingine zinazodhibitiwa na mawakala wa Wamarekani. Kwa sababu kila timu inataka kushinda kwa namna yoyote ile na hutumia ushawishi wao pale inapoongoza. Katika uchaguzi wa 2007, kila upande ulidai kushinda uchaguzi huo. Mapigano yalianza kati ya pande hizo mbili za mzozo, na damu ikatiririka, takriban watu 1,200 waliuawa, na mamia kwa maelfu walilazimika kuyahama makazi yao kutokana na

*Endelea... UK 11*

mashambulizi ya kikabila. Lakini katika suala hili, ujanja wa Kiingereza ulichangia kusitisha upinzani, hivyo uliweka mtego kwa kumpa Odinga nafasi ya uwaziri mkuu na Kibaki alibaki kuwa rais wa nchi, na mamlaka yote mkononi mwake, na kuweka vikwazo katika utekelezaji wa madaraka ya waziri mkuu. Lakini Kenyatta, ambaye alitangazwa ushindi wake katika uchaguzi wa 2013, alifuta wadhifa wa waziri mkuu ili kuchukua mamlaka yeye pekee. Katika uchaguzi wa 2017, upinzani ulidai udanganyifu na kutaka Mahakama ya Upeo kurudia uchaguzi huo. Uchaguzi ulirudiwa Oktoba 2017, na upinzani ukasusia, na Kenyatta na naibu wake, William Ruto, kutangazwa washindi. Pamoja na kujua kuwa Rais wa zamani wa Marekani Barack Obama aliingilia kati suala hilo kwa vile ana asili ya Kenya! Alitoa wito wa utulivu na kukubalika kwa matokeo ya uchaguzi, kwa sababu alijua kwamba uchaguzi ukifanyika, mawakala wa Uingereza watashinda tena, kwa sababu bado wangali wanaidhibiti dola hiyo, na kwa hili alitaka kupata baraka kwa watawala wa Kenya ili ushawishi wake kwao uwe na nguvu zaidi na hivyo kuimarisha ushawishi wa Amerika nchini Kenya na kutumia shinikizo ili mawakala wao wa baadaye waweze kufikia utawala. Lakini Uingereza ilikwepa mawakala wake kila mara ili kudumisha ushawishi wake wa vitisho nchini Kenya. Iliihadaa kupitia wakala wake Kenyatta kana kwamba inampenda wakala wa Marekani Odinga na kumfanya wakala wake Ruto ashinde.

5- Ni mara ya tano kwa Raila Odinga kutangaza kuwania kiti cha urais na kugombea na kushindwa katika uchaguzi. Hapo awali aligombea mara nne mnamo 1997, 2007, 2013 na 2017, lakini mawakala wa Uingereza wanaodhibiti ulingo wa kisiasa nchini Kenya hawakumwezesha kushinda. Alikuwa na matumaini ya kumrithi Uhuru Kenyatta, ambaye mihula yake miwili imekamilika na hawezi kuwania muhula wa tatu kwa mujibu wa katiba. Odinga na Kenyatta msuluhishi walisimama baada ya kupeana mikono Machi 9, 2018, baada ya miezi kadhaa ya mapigano ya umwagaji damu kati ya wafuasi wao, kutotambua ushindi wa Kenyatta na kujitangaza kuwa rais wa Kenya, na kwa kupeana mikono huku, kulitangazwa kumalizika kwa migawanyiko kati yao na kutambuliwa kwa urais wa Kenyatta. Odinga alimsifu Kenyatta kwa "hisia yake ya uzalendo katika kuanzisha mazungumzo ambayo yalisababisha kupeana mkono wa heri." Na wengine wakadhani wamefikia makubaliano ya kumtaka Odinga kumrithi Kenyatta, au Odinga amegeuka kuwa wakala wa Muingereza! Lakini Kenyatta na mawakala wa Uingereza hawakuhadaiwa na upatanisho huu, bali waliutumia kwa manufaa yao. Kenyatta alicheza mchezo wakati wa kampeni za uchaguzi kwa kuonyesha kwamba alimuunga mkono Odinga, akisema “Ruto hastahili na hafai kuchukua wadhifa wa juu zaidi nchini.” Ruto akajibu kwa kusema: “Hakika Kenyatta anataka amrithi ali awe rais kikaragosi”  (BBC 16/8/2022)

6- Inajulikana kuwa Chama cha Ruto kiliungana na Chama cha Kenyatta walipoafikiana mwaka wa 2012. Kisha, chama chao tawala kikapanuka, Chama cha Jubilee kikaundwa kutoka kwa muungano wa vyama 11 mnamo 9/8/2016 ili kushiriki uchaguzi wa 2017 na kiliongozwa na Kenyatta baada ya kuwa muungano wa kisiasa mwaka 2013 kumuunga mkono Kenyatta katika kampeni zake za uchaguzi. Ruto alikuwa mshirika na naibu katika vipindi vyote viwili, na alikuwa mfuasi wa wakala wa zamani wa Kiingereza, Rais wa zamani Daniel arap Moi, na alikuwa akihamasisha vijana kwa msaada wake, hivyo akapata kibali chake na kuanza kumpandisha vyeo serikalini. Ameshika nyadhifa za uwaziri akiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Kilimo na Waziri wa Elimu ya Juu. Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu ilimshtaki yeye pamoja na Kenyatta kwa kufanya uhalifu mwaka wa 2007 na 2008, na waliondolewa mashtaka na mahakama hiyo inayodhibitiwa na Ulaya. Kenyatta aliondolewa mashtaka mwaka wa 2014 na Ruto akaondolewa mashtaka 2016 ili kushiriki katika uchaguzi wa 2017 na kutangazwa ushindi wao ushindi ndani yake, huku Kenyatta akiwa rais na Ruto akiwa naibu wake. Kwa sababu hii, Ruto ni mmoja wa mawakala walioidhinishwa wa Waingereza, na hafikiriwi kuwa ataachiliwa kirahisi na nafasi yake kuchukuliwa na Odinga, wakala wa Amerika, kwa mujibu wa makubaliano hayo, isipokuwa ni hadaa tu iliyoratibiwa na ujanja wa Waingereza!

7- Kenyatta alizuru Uingereza kati ya 26 na 29/7/2021 na kukutana na Waziri Mkuu Johnson na kutangaza kuwa lengo la ziara hiyo ni "kuimarisha ushirikiano wa kimkakati kati ya Kenya na Uingereza" na pande hizo mbili zilitia saini makubaliano mapya ya ushirikiano wa ulinzi kwa miaka mitano. Alitangaza kuwa makubaliano hayo yanalenga "kuimarisha na kutilia nguvu ushirikiano kati ya nchi hizo mbili katika kukabiliana na changamoto za pamoja za usalama katika Afrika Mashariki" (BBC ya Uingereza). Uingereza haikufanya kama ilivyofanya Marekani na kuibua suala la Nyaraka za Pandora, masuala ya haki za binadamu na masuala ya ufisadi wakati Kenyatta alipoitembelea, haikufanya hivyo kwa sababu ya uaminifu na utii wake kwake! Kumbuka kuwa Uingereza ina kambi mbili za kijeshi nchini Kenya chini ya makubaliano kati ya nchi hizo mbili, mojawapo ikiwa karibu na Nairobi, mji mkuu wa Kenya, na dhamira yake ni kusaidia kuleta utulivu wa utawala nchini Kenya kwa manufaa ya ushawishi wa Uingereza na kuondoka kutoka huko hadi maeneo mengine kulinda ushawishi huu, na nyingine iko kaskazini mwa Kenya ambayo dhamira yake ni kutoa mafunzo kwa vikosi vya Uingereza vinavyojiandaa kupigana katika maeneo ya jangwa na nusu jangwa. Vikosi vya Uingereza vinafanya mazoezi katika eneo la nchi kavu sawa na mara nne yale ambayo jeshi la Uingereza hutumia katika nchi yake na silaha za moto na risasi zinazoiga hali halisi ya vita. Ripoti za vyombo vya habari zilisema kuwa wanajeshi wa Uingereza waliopigana nchini Afghanistan walikuwa wamefunzwa katika kambi hii nchini Kenya. Ndio maana Amerika inatilia maanani Kenya umuhimu mwingine kwa sababu ya uwepo wa misingi hii ya Kiingereza, kwani inafanya kazi ya kuiondoa kutoka huko.

8- Inaonekana Uingereza, wakati wa ziara ya Kenyatta kwao, ilimtaka aandae ziara ya Amerika ili kuwaonea huruma na kuthibitisha maridhiano na Odinga ili Marekani isifanye “matendo ya kuvuruga” uchaguzi unaokuja. Kwa hiyo, mipango ilikuwa ni kuzuru Amerika, na ndivyo ilivyokuwa baada ya takriban miezi miwili kutoka katika ziara yake nchini Uingereza, Rais Biden wa Marekani alimpokea Rais wa Kenya Uhuru Kenyatta mnamo 14/10/2021, na ndiye rais wa kwanza wa Afrika kupokewa

*Endelea... UK 12*

na rais wa Marekani. Msemaji wa Ikulu ya White House Jen Psaki alisema marais hao wawili watajadili "uhusiano thabiti wa nchi mbili pamoja na haja ya uwazi na uwajibikaji katika mifumo ya fedha ya ndani na kimataifa." Jina la Kenyatta lilitajwa katika uchunguzi wa "Nyaraka za Pandora" uliofanywa na Muungano wa Kimataifa wa Wanahabari wa Uchunguzi juu ya kupambana na ufisadi, yeye pamoja na watu sita wa familia yake wanamiliki kwa siri mtandao wa makampuni 11, ambayo moja inamiliki hisa zenye thamani ya dolari milioni thelathini. Akijibu taarifa hiyo Psaki aliongeza kusema "Rais siku zote amekuwa akikemea mambo yasiyolingana (matumizi mabaya) katika mfumo wa fedha wa kimataifa, hii haimaanishi kuwa hatutakutana na watu tunaotofautiana nao, kuna masuala kadhaa ambayo tunayo nia ya kufanya kazi na Kenya na hilo ndilo litakalokuwa lengo kuu [la mkutano kati ya marais hao wawili.) Marais hao wawili watajadili juhudi za kutetea demokrasia na haki za binadamu, kuendeleza amani na usalama, kuharakisha ukuaji wa uchumi na makubaliano na mabadiliko ya tabianchi" (AFP 14/10/2021).

Amerika ilijaribu kutumia nyaraka hizo kutia shinikizo kwa Kenyatta kutangaza kuunga mkono ugombezi wa Odinga, ilifanya hivyo na akaonekana ni mfuasi wa Odinga, lakini uungwaji mkono huu haukuwa wa dhati, bali ni wa kinafiki ili kuficha kashfa zake ili Marekani isiwachokoze na kumchafua, hivyo ilikuwa vigumu kwake kugombea kwa muhula wa tatu na Amerika ilitikisa upinzani wake kwa mfano huo... Mnamo Novemba 17, 2021 Waziri wa Mambo ya Nje wa Amerika alizuru Kenya kama sehemu ya ziara yake ya Afrika iliyojumuisha pia Nigeria na Senegal, ambayo ilidumu kwa wiki moja. Alisema alipokuwa katika mji mkuu wa Nigeria: "Serikali zimekuwa na uwazi mchache,". Hili linafanyika kote barani Afrika. Viongozi wanapuuza mipaka ya utawala, wizi au kuahirisha uchaguzi, kutumia malalamiko ya kijamii ili kupata na kudumisha mamlaka, kukamata viongozi wa upinzani, kukandamiza vyombo vya habari na kuruhusu huduma za usalama kuweka vikwazo vya kikatili kwa janga la maambukizi (Korona)" (Asharq Al-Awsat 21/11/2021).

Vile vile, misingi ya chama cha Kenyatta ilikuwa ikifanya kazi ya kutafuta uungwaji mkono kwa Ruto, huku makubaliano ya ndani ya chama yakiwa miongoni mwa mawakala walioujua mchezo huo na kumchagua Ruto licha ya kujifanya kumpinga.

9- Nchi nyingi za Afrika chini ya ushawishi wa Ulaya, ikiwa ni pamoja na Kenya na Senegal, zinafanya kazi ya kuimarisha China dhidi ya Amerika, ambayo inajitahidi kupanua ushawishi wake ndani yake. Senegal, chini ya ushawishi wa Ufaransa, inaimarisha uhusiano wake na China. Ilikuwa mwenyeji wa Jukwaa la Ushirikiano wa China na Afrika katika mji mkuu wake, Dakar, kati ya Novemba 29 na 30/11/2021, na Waziri wa Mambo ya Nje wa Senegal Isata Tal Sal alisema, "Tuna diplomasia huru, ambayo hatuzuii mtu yeyote." Wakati ushawishi wa Amerika barani Afrika, bado ni mdogo tofauti na ushawishi wa Uingereza na Ufaransa, inafanya kazi ya kuimarisha kwa njia na kazi mbalimbali Ili kushindana na ushawishi wa kiuchumi wa China ambao Uingereza na Ufaransa zinaimarisha ili kuimarisha mawakala wao barani Afrika. Hivi majuzi, Diwani wa Jimbo la China na Waziri wa Mambo ya Nje, Wang Yi alizuru Kenya mnamo 6/1/2022, na kukutana na Rais Kenyatta, ambaye alisema: "China sio tu rafiki wa dhati wa Kenya, bali pia ni mshirika wa maendeleo wa ushirikiano wa karibu... mafanikio ya maendeleo hayataweza kupatikana bila uungaji mkono mkubwa wa China... Kenya inapenda kuzidisha ushirikiano wa kunufaishana na China ili kufikia maendeleo ya pamoja," huku Waziri wa Mambo ya Nje wa China Wang Yi akisema, "China inapenda kuimarisha ushirikiano wa pande mbili pamoja na Kenya kuisaidia kuimarisha uwezo wake wa kujiendeleza, kuharakisha ukuaji wa viwanda na kukuza Mshikamano na uratibu nayo katika masuala ya kimataifa na pande nyingi." Wang aliwasilisha "Mpango wa Maendeleo Salama katika Pembe ya Afrika." Kenyatta alisema, "Mpango huu unakidhi mahitaji ya dharura ya nchi za Pembe ya Afrika, na Kenya inakubali kucheza dori katika suala hili" (Xinhua 6/1/2022). Haya yote yanaikasirisha Amerika, ambayo inajitahidi kudhoofisha ushawishi wa Ulaya barani Afrika na pia kufanya kazi kupunguza nguvu inayokua ya China.

10- Mukhtasari ni kwamba ushawishi wa Uingereza bado una nguvu nchini Kenya na wengi wa wahusika wa kisiasa ni miongoni mwa mawakala wake, huwaunganisha haja inapotokea na pia huwagawanya inapobidi. Iwapo hapana budi kuwepo na makubaliano kati ya mawakala wake na mawakala wa Marekani, na kisha kugawanya mamlaka pamoja nao huku ikishikilia udhibiti, inafanya hivyo na kuwaagiza wateja wake kupatanisha na kuhitimisha makubaliano katika suala hili. Na ikiwa itafaulu kumweka wakala wake Ruto madarakani na akafanikiwa kunyamazisha upinzani, basi hatamwagiza wakala wake kufanya hivyo, kwa kuwa wako mikononi mwake na wanatafuta tu mamlaka, kwa namna ya mawakala wa Marekani. Hii ndio desturi ya mawakala katika kila nchi. Kwa upande wa Amerika, haitaondoka uwanjani na itafanya kazi ya kuimarisha ushawishi wake nchini Kenya, na haipendezwi na umwagaji damu, machafuko na ghasia ndani yake na katika nchi zingine za Kiafrika. Inafanya kazi kwa mitindo na mbinu mbalimbali, iwe ni za kiuchumi, kisiasa, au katika ngazi ya usalama na kijeshi. Inafanya kazi ya kuvuna mawakala katika sekta hizi mbili kwa jina la uwekezaji wa usalama na kusaidia kutoa mafunzo kwa jeshi na vikosi vya usalama, na kisha inafanya kazi ya kuandaa mapinduzi kama ilivyofanya nchini Mali au kuchochea uasi kama ilivyokuwa nchini Chad, uasi huo ulisababisha kuuawa kwa wakala wa Ufaransa, Idriss Deby.

Kwa hivyo, nchi hizi, nyingi zao zikiwa ni nchi za Kiislamu, zimesalia kuwa uwanja wa mvutano wa kimataifa, haswa kati ya Amerika, Uingereza na Ufaransa. Hakuna matumaini kwa nchi hii kuondokana na mvutano huu wa kikoloni unaoifanya kuwa nyuma na ilhali ni miongoni mwa nchi tajiri zaidi kwa rasilimali, isipokuwa kwa kurudi Khilafah kwa njia ya Utume. Mtume wa Mwenyezi Mungu (saw) ametoa bishara njema ya kusimama kwake kwa kusema:

«ثُمَّ تَكُونُ خِلَافَةٌ عَلَى مِنْهَاجِ النُّبُوَّةِ»

**"Kisha itakuwepo Khilafah kwa njia ya Utume."**
Imepokewa na Ahmad.

**1 Safar 1444 H**
**28/8/2022 M**